



**NAETISL**

National Association of  
Educational Translators and  
Interpreters of Spoken Languages



**MODDC**

Missouri  
Developmental  
Disabilities Council

# Mikutano ya IEP inayoongozwa na Wanafunzi: Mwongozo wa Mzazi

---

Funding for the Supporting Language Access in Schools Project in Missouri provided by the Missouri Developmental Disabilities Council, was supported by the Administration for Community Living (ACL), U.S. Department of Health and Human Services (HHS) as part of a financial assistance award totaling \$1,361,246 with 100 percent funding by ACL/HHS. The contents are those of the author(s) and do not necessarily represent the official views of, nor an endorsement, by ACL/HHS, or the U.S. Government.



[naetisl@gmail.com](mailto:naetisl@gmail.com)

NAETISL



*Follow us*



MODDC



[moddc@moddcouncil.org](mailto:moddc@moddcouncil.org)



[www.naetisl.org](http://www.naetisl.org)

[www.moddcouncil.org](http://www.moddcouncil.org)





## Mikutano ya IEP inayoongozwa na Wanafunzi: Mwongozo wa Mzazi

### **Je, Mkutano wa IEP unaoongozwa na mtoto ni gani?**

Ni mkutano wa Mpango wa Elimu ya Kibinafsi (IEP) ambapo mwanafunzi anaongoza katika kupanga elimu yake mwenyewe. Badala ya watu wazima kuongoza mazungumzo, wanafunzi hushiriki kikamilifu na wakati mwingine huongoza sehemu za mkutano wenyewe.

### **Umuhimu wa wanafunzi kuongoza mikutano yao ya IEP ni gani?**

Wanafunzi wanapoongoza, wanajifunza kujitetea (kujitetea) na kufanya maamuzi kuhusu siku zao za usoni (kujitawala). Hii inaweza kuwasaidia kufaulu shuleni na kujiandaa kwa kazi ama vyuo vikuu baada ya kuhitimu.

### **IEP inayoongozwa na mwanafunzi na ile ya kawaida zina tofauti gani?**

Katika mikutano ya kawaida, wanafunzi kwa kawaida huzungumza takriban 3% tu ya wakati. Katika mikutano inayoongozwa na wanafunzi, mwanafunzi hushiriki zaidi, husaidia kuongoza maamuzi, na huchukua jukumu kubwa badala ya kuwa mshiriki aliyenyamaza.

### **Je, wanafunzi wote wanaweza kushiriki kwenye IEP zinazoongozwa na wanafunzi?**

Ushiriki unaweza kurekebishwa kulingana na umri wa mwanafunzi, mahitaji yake, na uwezo wake. Wanafunzi wachanga wanaweza tu kushiriki kazi zao au kuzungumza kuhusu kile wanachofurahia kujifunza. Wanafunzi wakubwa wanaweza kuongoza mkutano mzima na kusaidia timu kufanya maamuzi.





## Je, mwanafunzi anaweza kujiandaa aje kuongoza mikutano yake ya IEP?

Maandalizi ni muhimu. Waalimu na wazazi wanaweza kuwasaidia wanafunzi:

- Kujielewa wenyewe: kile wanachofanya vizuri, changamoto wanazopitia, na jinsi ulemavu wao unavyoathiri masomo.
- Kuelewa mpango wao wa IEP: kile unachosema na haki zao.
- Kupanga ule mkutano: kufanya mazoezi ya watakachokisema, kuunda ajenda, na kujiandaa kwa maswali. Wanaweza pia kutumia mawasilisho au teknolojia nyingine kusaidia.

## Wazazi wana jukumu gani katika mikutano ya IEP inayoongozwa na wanafunzi?

Wazazi wanaweza kusaidia kwa:

- Kuongea na Watoto wao kuhusu ile IEP na mchakato wa mkutano.
- Kuwatia moyo Watoto wao kuongoza sehemu au mkutano mzima.
- Kuendeleza mawasiliano na waalimu na wafanyakazi wa shuleni kuunga mkono kuhusika kwa mwanafunzi.

## Je, mikutano ya IEP inayoongozwa na wanafunzi inaweza kubadilika?

Hakuna njia moja ya kufanya ile mikutano. Kila mwanafunzi anaweza kushiriki kwa njia inayolingana na uwezo wake na kiwango cha faraja, kutoka kushiriki kidogo hadi kuongoza mkutano kamili.

## Je, ni faida gani za muda mrefu za mikutano ya IEP inayoongozwa na wanafunzi?

Wanafunzi wanaoshiriki kikamilifu huwa na ari zaidi, ujasiri, na ujuzi wa kujitetea. Ujuzi huu huwasaidia shuleni, kazini, na maishani baada ya kuhitimu.

